JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA

HOTUBA YA MHE. BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB.),
WAZIRI WA FEDHA, AKIWASILISHA BUNGENI
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI
KWA MWAKA 2025/26 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO
NA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27.



DODOMA

2 JUNI 2026

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# HOTUBA YA MHE. BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB,), WAZIRI WA FEDHA, AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

**2 JUNI 2026**

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26 inayojumuisha mafungu tisa (9) ambayo ni Fungu 001 – Deni la Serikali; Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 013 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; Fungu 021 – Hazina; Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu; Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 050 – Wizara ya Fedha; na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Aidha,

ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya mafungu manane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2026/27.

## 1.1 Shukrani na Pongezi

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha, kwa mara ya kwanza, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 29, 2025 na kumwezesha kupata fursa nyingine ya kuliongoza Taifa letu kwa kipindi cha miaka mitano. Kuchaguliwa kwake ni ishara ya imani kubwa waliyonayo wananchi kwa Mheshimiwa Rais. Ninamuombea Mheshimiwa Rais afya njema na utekelezaji mwema wa majukumu yake.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumpongeza Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nampongeza kwa

kazi kubwa na adhimu anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya kuliongoza Taifa letu. Aidha, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, naye kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuiongoza tena Zanzibar kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** (Mb,), kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawaombea viongozi wetu wote afya njema na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yao.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninampongeza pia kwa Hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa bungeni, ambayo imetoa Dira na Mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2026/27. Hotuba hiyo imeeleza kwa kina mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha mwaka 2025/26, Mipango ya Serikali kwa mwaka 2026/27 pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Ninaahidi kuwa, nitasimamia kikamilifu utekelezaji wa masuala yote yanayohusu Wizara ya Fedha kama yalivyoainishwa katika Hotuba hiyo.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa muhimili wetu huu wa kutunga Sheria, ninaomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe

binafsi Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb,), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb,), Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu kuliongoza Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga - Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika – Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe kuliongoza Bunge lako Tukufu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia**

**Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti katika mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa lengo la kukuza uchumi na kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi. Kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge hili la 13 na pia kwa kuniteua kumsaidia kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwateua Mheshimiwa *Mhandisi* Mshamu Ali Munde (Mb,) na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula (Mb,) kuwa Naibu Mawaziri na wasaidizi wangu. Mimi binafsi pamoja na wasaidizi wangu na wataalamu wa Wizara wakiongozwa na Dkt. Natu El-maamry Mwamba, tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzetu kuwa tutatekeleza

kikamilifu majukumu yetu ili kufikia malengo na shabaha zilizoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 wa utekelezaji wa DIRA 2050. Tunamwombea Mhe. Rais afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra, mifumo na mwelekeo wa Taifa letu kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya Watanzania.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati ya moyo wangu, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Mashariki na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kwa uongozi thabiti wa Kamati. Aidha, ninawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa

mashirikiano yao makubwa na kwa kupokea, kuchambua na kujadili kwa kina na uwazi Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26 na kupitisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2026/27. Maoni na ushauri wao umekuwa na tija katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**9.** ***Mheshimiwa Spika*****,** ninawashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia mimi binafsi, manaibu wangu na Wizara kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa niaba ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, ninalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa kwa upande wetu, tutaendelea kutimiza wajibu wetu wa kutoa ushirikiano na

kufanya kazi kwa pamoja ili huduma bora na stahiki ziwafikie wananchi wote na kwa wakati.

### 1.2 Salamu za Pole

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa huzuni na majonzi, natumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge, familia, ndugu na jamaa kwa kuondokewa na Wapendwa wetu: Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kilichotokea Machi 25, 2026; Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na aliyewahi kuwa waziri

katika Wizara mbalimbali, kilichotokea Desemba 11, 2025; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mwakilishi wa Wafanyakazi kutoka Vyama vya Wafanyakazi aliyefariki dunia Januari 18, 2026. Taifa limepoteza viongozi mahiri ambao walikuwa na mchango mkubwa katika nafasi zao za uongozi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo yangu ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hoja iliyo mbele yetu kwa mjadala na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni: Muhtasari wa Majukumu ya Wizara; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi

ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 686 la Desemba 19, 2025 pamoja na Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara ulioidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Machi 12, 2026. Majukumu ya msingi ya Wizara ni pamoja na: kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya usimamizi wa bajeti ya Serikali; kusimamia uchumi; kusimamia ukusanyaji wa

mapato ya Serikali; kusimamia na kuratibu upatikanaji wa fedha za nje na kuimarisha mahusiano na taasisi za fedha za kikanda na kimataifa.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine ya Wizara ni: kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu; kusimamia mali za Serikali; kusimamia shughuli za ukaguzi wa ndani na nje; kusimamia mali za adui; kusimamia deni la Taifa, mikopo, misaada na dhamana; kusimamia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar; kusimamia maendeleo ya masoko ya mitaji na bidhaa; kusimamia takwimu rasmi za kitaifa; kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha; kuboresha utendaji na maendeleo ya

rasilimaliwatu katika Wizara; kusimamia idara zinazojitegemea, mashirika ya umma, wakala za Serikali, na taasisi zilizo chini ya Wizara; na kusimamia programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na taasisi zilizochini yake.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

### 3.1 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, mafungu manane (8) ya Wizara ya Fedha yalipitishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 20,176.10 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 19,428.80 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara

shilingi bilioni 1,101.59 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 18,327.21. Aidha, bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 747.30 ikijumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 601.70 na fedha za nje shilingi bilioni 145.60.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti, bajeti ya mafungu manane (8) ya Wizara ilihuishwa na kupungua kutoka shilingi bilioni 20,176.10 hadi shilingi bilioni 19,940.16. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 19,454.16 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 485.99 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi bilioni 18,672.87 na mishahara shilingi bilioni 781.29 Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za

ndani shilingi bilioni 429.52 na fedha za nje shilingi bilioni 56.47.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwisho wa Aprili 2026, jumla ya fedha zilizopokelewa na mafungu manane (8) ya Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi bilioni 14,083.11, sawa na asilimia 70.63 ya bajeti iliyohuishwa. Aidha, matumizi halisi yalifikia shilingi bilioni 14,049.76, sawa na asilimia 99.76 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi yalikuwa shilingi bilioni 13,099.71, mishahara shilingi bilioni 534.76 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 415.29.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipitishiwa bajeti ya shilingi bilioni 122.52 kwa mwaka 2025/26 kwa ajili ya

matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 110.42 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 12.10, kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi bilioni 87.36 na mishahara shilingi bilioni 23.06. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 8.83 na fedha za nje shilingi bilioni 3.28.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwisho wa Aprili 2026, Fungu 045 limepokea jumla ya shilingi bilioni 118.92, sawa na asilimia 97.06 ya bajeti iliyoidhinishwa. Matumizi halisi yalifikia shilingi bilioni 110.93, sawa na asilimia 93.28 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa shilingi bilioni 84.59, mishahara shilingi bilioni 18.03 na shilingi bilioni 8.32 kwa ajili ya matumizi ya

maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa na kutumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.1 – 3**.

### 3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2025/26

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutekeleza jumla ya vipaumbele vitano (5) ambavyo ni: kutafuta na kukusanya rasilimali fedha shilingi bilioni 50,181.55 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali; kuhudumia kwa wakati deni la Serikali linalotarajiwa kuiva la jumla ya shilingi bilioni 14,219.35; kujenga mfumo wa pamoja wa kutoa ankara za malipo ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; kuboresha, kuunganisha na

kuimarisha usalama wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha na mali za umma; na kuandaa Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma. Hadi Aprili 2026, utekelezaji wa vipaumbele umefikia hatua zifuatazo:

### 3.2.1 Kukusanya Mapato, Kutafuta Misaada na Kugharamia Nakisi ya Bajeti ya Serikali

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, mafungu ya Wizara ya Fedha yalikadiriwa kukusanya na kutafuta shilingi bilioni 50,181.6 kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ikiwa ni asilimia 88.8 ya bajeti ya Serikali ya jumla ya shilingi bilioni 56,490.30. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya na kutafuta jumla ya shilingi bilioni 41,373.2 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 82.4 ya lengo la

mwaka. Kiasi hicho kimegawanyika kama ifuatavyo:

### (a) Mapato ya Ndani

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni 34,157.4. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 34,103.9 na Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 53.5. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya mapato yaliyopatikana ni shilingi bilioni 29,345.1, sawa na ufanisi wa asilimia 85.9 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, mapato halisi yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 29,319.6, sawa na asilimia 86.0 ya lengo la mwaka, na Wizara ilikusanya maduhuli ya shilingi bilioni 25.5, sawa na ufanisi wa asilimia 47.6 ya lengo

la mwaka. Ukusanyaji wa mapato ya kodi ulifikia ufanisi wa asilimia 105.1 ya lengo la kipindi cha marejeo. Mafanikio hayo, yamechangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini, maboresho ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, kuongezeka kwa kiwango cha uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari, kuimarika kwa mifumo ya ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi, na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara.

**(b)Misaada**

**22.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilikadiriwa kutafuta misaada ya jumla ya shilingi bilioni 925.1 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi Aprili 2026, Wizara ilifanikiwa kutafuta na kupokea misaada ya jumla ya

shilingi bilioni 740.5, sawa na ufanisi wa asilimia 80.0 ya lengo la mwaka.

### (c) Kugharamia Nakisi ya Bajeti ya Serikali

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilikadiriwa kutafuta mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 15,099.1. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,539.7 ni mikopo ya ndani na shilingi bilioni 9,559.4 ni mikopo ya nje. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya shilingi bilioni 11,287.5 zilipatikana kupitia mikopo ya ndani na nje, ambapo mikopo ya ndani ya kibiashara ilikuwa shilingi bilioni 5,083.8, sawa na ufanisi wa asilimia 91.8 ya lengo la mwaka, mikopo ya nje ya kibiashara ilikuwa shilingi bilioni 1,590.3, sawa na ufanisi wa asilimia 60.5 ya lengo la mwaka la kukopa shilingi bilioni 2,629.0. Aidha, mikopo ya nje yenye masharti nafuu ilifikia shilingi bilioni

4,613.4, sawa na ufanisi wa asilimia 66.6 ya lengo la mwaka la kukopa shilingi bilioni 6,930.4.

### 3.2.2 Kuhudumia Deni la Serikali

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kulipa kwa wakati deni la Serikali lililotarajiwa kuiva la jumla ya shilingi bilioni 14,219.4. Hadi Aprili 2026, jumla ya shilingi bilioni 9,737.7, sawa na asilimia 68.5 ya lengo la mwaka zimepokelewa na kutumika kulipa deni lililoiva. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,445.1 zimetumika kulipa deni la nje na shilingi bilioni 5,292.6 zimetumika kulipa deni la ndani. Ufanisi katika ulipaji deni lililoiva, umeiwezesha nchi yetu kuendelea kuaminika katika masoko ya fedha ya kikanda na kimataifa. Nina furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imeibuka mshindi wa

jumla katika Tuzo ya Usimamizi wa Deni la Umma katika nchi za Jumuiya ya Madola, pamoja na tuzo ya Ofisi Bora ya Usimamizi wa Deni la Serikali katika Kanda ya Afrika.

### 3.2.3 Kujenga Mfumo wa Pamoja wa Kutoa Ankara za Malipo ya Serikali

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kujenga Mfumo wa Pamoja wa Kutoa Ankara za Malipo ya Serikali (*Universal Billing System*) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Hadi Aprili 2026, Wizara imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mfumo na awamu ya pili ujenzi wake umefikia asilimia 70. Kukamilika na kuanza kutumika kwa Mfumo huo kutaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, hususan tozo na ada pamoja na kupunguza gharama za uwekezaji na biashara kwa sekta binafsi.

### 3.2.4 Kuboresha, Kufungamanisha na Kuimarisha Usalama wa Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kufungamanisha Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) na Mfumo wa Bima ya Afya (ERMS-NHIF), Mfumo wa Malipo ya Wastaafu Wanaolipwa na Hazina (TPPS), Mfumo wa Usimamizi wa Wanachama (MAS - PSSSF) pamoja na mifumo ya benki za biashara ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wafanyakazi na wastaafu. Hadi Aprili 2026, Mfumo wa TPPS umefungamanishwa na mifumo ya benki nane (8) za biashara na Mfumo wa MAS (PSSSF). Aidha, Mfumo wa MUSE umeunganishwa na Mfumo wa Ununuzi wa Umma - NeST ili kurahisisha malipo katika ununuzi wa umma na mikataba husika

kusimamiwa moja kwa moja kupitia Mfumo wa MUSE.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa MUSE umeboreshwa kwa kuongeza moduli ya kulipa moja kwa moja kwenye mitandao ya simu ambapo imerahisisha malipo kwa walengwa ambao hawawezi kupata huduma za benki kwa urahisi na imepunguza gharama kwa wananchi, hususan waishio vijijini. Aidha, Mfumo huu unatumika kulipa wahudumu wa afya ngazi ya jamii na kulipa malipo ya kifuta machozi kwa wananchi wanaopata madhara kutokana kuingiliwa na wanyama wakali na waharibifu wa mali.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na eGA imeendelea kuimarisha usalama wa mifumo ya kifedha dhidi ya

mashambulizi ya kimtandao kwa kuongeza sifa au vipengele mahsusi vya utambuzi wa watumiaji wa mifumo, kufanya kaguzi za mara kwa mara, na kuimarisha udhibiti wa upatikanaji wa mifumo na taarifa muhimu za kifedha. Aidha, Wizara imeimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa matukio ya kiusalama kwa kutumia teknolojia za kisasa za kubaini na kuzuia mashambulizi ya kimtandao, kutoa mafunzo ya uelewa wa usalama wa mitandao kwa watumishi, na kushirikiana na taasisi za uthibiti katika kukabiliana na vihatarishi vya kimtandao vinavyoweza kuathiri huduma za fedha zinazotolewa na Wizara.

#### 3.2.5 Kuandaa Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuandaa Sera ya Usimamizi wa

Mali za Umma kwa lengo la kuweka mwongozo wa kisera wa usimamizi na uratibu wa matumizi ya mali za umma. Hadi Aprili 2026, Wizara imekamilisha mchakato wa kukusanya taarifa kutoka kwa wadau, kufanya tathmini ya mahitaji na kuandaa rasimu ya awali ya Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma pamoja na Mikakati ya Utekelezaji na Mawasiliano itakayowasilishwa kwa wadau mara mchakato wa kuidhinisha Sera utakapoanza Julai 2026.

## 3.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

### 3.3.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara iliendelea na kazi ya kubuni na kutekeleza sera ya fedha na bajeti ili kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu. Shabaha za uchumi jumla zilizobuniwa ni ukuaji

wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.5 mwaka 2024; akiba ya fedha za kigeni kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne; nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa; kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa; na mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo ya uchumi jumla, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kiutendaji ikiwa ni pamoja na kuhudumia kwa wakati deni la Serikali lililokuwa limeiva la jumla ya shilingi bilioni 9,737.7; kununua tani 17.64 za dhahabu zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2,616.77

na kufikisha tani 24.21 za akiba ya dhahabu zenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,591.39; kuchochea ukuaji wa asilimia 20.2 wa mikopo kwa sekta binafsi; kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa mpango wa muda wa kati wa ukopaji ambapo mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 11,287.5 imepatikana na kuelekezwa kwenye uwekezaji na malipo ya hatifungani zilizoiva; kudhibiti mzunguko wa fedha katika soko uliosaidia mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3.0 na 5.0; na kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ya jumla ya shilingi bilioni 667.29.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na hatua hizo za kisera na kiutendaji zilizotekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma na binafsi, Pato la Taifa kwa mwaka

2025 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.9 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi, kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, kuimarika kwa shughuli za kilimo, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na shughuli za ujenzi wa umma na binafsi pamoja na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na huduma za jamii. Shughuli za fedha na bima ziliongoza kwa ukuaji wa asilimia 15.7 ikifuatiwa na shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme na gesi asilimia 11.8, uchimbaji madini na mawe asilimia 9.4, habari na mawasiliano asilimia 8.8, sanaa na burudani asilimia 8.5 na usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 8.0.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa viashiria vingine vya uchumi, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 unaonesha kuwa mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa za vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo katika masoko ya nchi jirani. Hata hivyo, kiwango cha mfumuko wa bei kimeendelea kuwa ndani ya lengo tulilojiwekea ndani na kikanda. Aidha, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,722.5, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.4. Hii ni juu ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi cha angalau miezi minne (4). Vilevile, ukusanyaji wa mapato ya

kodi umeendelea kuwa zaidi ya asilimia 100 ya lengo la kila mwezi na mpango wa ukopaji kutoka vyanzo vya kibiashara vya ndani na nje kuendelea kutekelezwa kama ulivyopitishwa na Bunge.

### 3.3.2 Kusimamia Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma Sura 348, Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 ili kuimarisha usimamizi wa bajeti ya Serikali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, ridhaa ya matumizi iliyotolewa bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni ilikuwa shilingi bilioni 40,920.2 sawa na asilimia 98.8 ya

lengo la kipindi husika. Kati ya kiasi hicho, mishahara na stahiki za watumishi ni shilingi bilioni 7,017.5, gharama za bidhaa na huduma shilingi bilioni 7,023.5, malipo ya riba shilingi bilioni 5,088.9, ruzuku, michango, mafao, misaada ya kijamii na gharama nyingine shilingi bilioni 19,410.6 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 2,379.7.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** utolewaji wa fedha ulizingatia maeneo ya vipaumbele ikiwa ni pamoja na ugharamiaji wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, huduma ya deni la Serikali, mishahara, mahitaji ya sekta ya hifadhi ya jamii na ujenzi wa miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji ili kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kuimarisha ustawi wa maisha ya wananchi. Aidha, Wizara iliandaa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango

na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) na kuipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 3.3.3 Usimamizi wa Mali za Serikali

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuhakiki mali za umma katika taasisi na vituo 275 vya Serikali, kuondosha kwa asilimia 100 mali chakavu, sinzia na ziada zilizoidhinishwa katika taasisi za umma na kuwezesha matumizi ya mfumo wa kielekitroniki wa usimamizi wa mali za umma (GAMIS) kwa taasisi 612. Hadi Aprili, 2026, Wizara ilifanya uhakiki wa mali za umma katika taasisi na vituo 245, uhakiki wa uhamisho wa mali katika vituo 10 na uhakiki wa miundombinu ya kuhifadhia fedha katika taasisi za umma 106. Aidha, vibali 121 kati ya vibali 167 vya

kuondosha mali vilivyotolewa vimetekelezwa, sawa na asilimia 72.46 ambapo mali zenye thamani ya shilingi bilioni 6.25 zimeondoshwa. Vilevile, taasisi za umma 644 zimewezeshwa kutumia mfumo wa GAMIS ambapo mali 4,159,971 zenye thamani ya shilingi trilioni 39.2 zimesajiriwa kwenye Mfumo.

### 3.3.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kufanya mapitio na kutoa ushauri kwa miradi 20 ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kuendesha mikutano sita (6) ya uhamasishaji kuhusu Sera ya Taifa ya PPP ya Mwaka 2009; kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya PPP; kufanya mapitio ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; kuandaa Mwongozo wa Ahadi za

Kibajeti na Madeni Sanjari yanayotokana na utekelezaji wa miradi ya PPP; na kutoa mafunzo kuhusu dhana na Sheria ya PPP. Hadi Aprili 2026, Wizara ilifanya mapitio na kutoa ushauri kwa miradi mitano (5) ambayo ni: Mradi wa Usalama Barabarani Tanzania; Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto; Mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (awamu ya pili, ya tatu na ya nne); Ujenzi wa Barabara ya Haraka ya Tozo kipande cha Kibaha - Mlandizi - Chalinze - Morogoro; na Ujenzi na Uendeshaji wa Jengo la Biashara na Hoteli ya Nyota Nne katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere, Dar es Salaam.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya PPP ya Mwaka 2009 ambapo taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera imeandaliwa. Aidha, Wizara imefanya

mapitio ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kuandaa maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho na kuyawasilisha kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni. Vilevile, Mwongozo wa Ahadi za Kibajeti na Madeni Sanjari yanayotokana na utekelezaji wa miradi ya PPP umeandaliwa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia iliendesha mikutano minne (4) ya uhamasishaji kuhusu Sera ya Taifa ya PPP ya mwaka 2009 na mikutano mitatu (3) kuhusu Sheria na Kanuni za PPP kwa taasisi za umma na wananchi. Wizara iliwajengea uwezo wadau 1,800 kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu namna ya kutambua na kuchambua miradi inayofaa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

### 3.3.5 Kusimamia Ununuzi wa Umma na Ugavi

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuimarisha mfumo wa usimamizi wa ununuzi wa umma na ugavi nchini ikiwemo: kuzindua rasmi Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025; kufanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kwa lengo la kuiwianisha na matakwa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi Endelevu; kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Umma, Wataalamu na Wazabuni wanaojihusisha na shughuli za ununuzi wa

umma na ugavi; kutoa mafunzo kwa watumishi wa kada ya ununuzi na ugavi kuhusu mnyororo wa ugavi endelevu; pamoja na kufanya tathmini ya kina kuhusu ushiriki wa makundi maalum ya kijamii, kampuni za ndani na wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs) katika utekelezaji wa shughuli za mnyororo wa ugavi.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 imezinduliwa rasmi; na Mkakati wa Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi Endelevu umekamilika. Aidha, Wizara imekamilisha tathmini ya ushiriki wa makundi maalum ya kijamii, kampuni za ndani pamoja na wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs) katika shughuli za mnyororo wa ugavi. Matokeo ya tathmini hiyo yamejumuishwa katika mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya

Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, ili kuhakikisha kuwa makundi haya yanapata fursa stahiki na shirikishi katika soko la ununuzi wa umma na ugavi. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kwa jumla ya watumishi 209 wa kada ya ununuzi na ugavi kutoka Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchi nzima, kuhusu usimamizi wa mnyororo wa ugavi endelevu.

### 3.3.6 Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutathmini na kusimamia udhibiti na uwajibikaji wa matumizi ya fedha na mali za umma; kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi, na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma; na kuboresha mfumo wa ukaguzi wa ndani kutoka mfumo wa kawaida hadi mfumo

wa ukaguzi wa kielektroniki. Hadi Aprili 2026, tathmini ya ubora wa vitengo vya ukaguzi wa ndani ilifanyika katika taasisi za umma 310 na kamati za ukaguzi katika taasisi za umma 36. Mafunzo yametolewa kwa wakaguzi wa ndani 150 kutoka taasisi za umma 226 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani (GIAMIS) na wakaguzi wa ndani 120 kuhusu ukaguzi wa athari za mabadiliko ya tabianchi na ustahimilivu wa majanga. Aidha, wakaguzi wa ndani 225 wamejengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Kukusanya Mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (TAUSI) na taasisi za umma 230 zimewezeshwa kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (GERMIS). Vilevile, wakaguzi wa ndani 228 kutoka taasisi za umma 157 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi na uandishi wa taarifa pamoja na ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA.

### 3.3.7 Kuimarisha Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuwezesha utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uendelevu na Maandalizi ya Taarifa Jumuishi ya Uendelevu (*IFRS Sustainability Standards 1 & 2*), kujenga uwezo wa wahasibu wa Serikali kuhusu viwango vipya vya kimataifa vya uhasibu (IPSASs), na kutoa msaada wa kitalaamu katika utekelezaji wa IPSAS 41 ili kuboresha usimamizi wa fedha za umma. Hadi Aprili 2026, Wizara imetoa msaada wa kitalaamu kwa taasisi za umma 609 katika maandalizi ya Moduli ya Hasara Tarajiwa (*ECL Model - IPSAS 41*) na kutoa mafunzo kuhusu uandaaji wa hesabu kulingana na viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa wahasibu na maafisa usimamizi wa fedha kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa

184. Aidha, mafunzo kwa vitendo kuhusu uandaaji wa taarifa za uendelevu yalitolewa kwa watumishi 91 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, mafunzo kuhusu matumizi ya viwango vya uendelevu na viwango vipya vya kimataifa vya uhasibu (IPSASs) yalitolewa kwa wahasibu 300 kutoka taasisi za umma.

### 3.3.8 Huduma za Mafao ya Kustaafu, Pensheni na Mirathi

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina pamoja na maslahi yao, na kuimarisha usimamizi wa mafao ya wastaafu, mafao ya vifo na michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Hadi Aprili 2026, Wizara

imeongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,125.87 hadi shilingi 250,000 na kulipa kwa wakati mafao ya wastaafu kiasi cha shilingi bilioni 577.41 baada ya kupokea majalada kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, michango ya kila mwezi ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ya shilingi bilioni 1,428.05 ililipwa kama ilivyopangwa.

### 3.3.9 Kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Fedha

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuandaa miongozo na kanuni za usimamizi wa sekta ya fedha; kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miongozo ya usimamizi wa huduma ndogo za fedha; na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi wa mifuko na programu za

uwezeshaji wananchi kiuchumi. Hadi Aprili 2026, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 umeandaliwa na kusomwa kwa mara ya kwanza bungeni. Aidha, Wizara ilitoa elimu ya huduma za fedha kwa umma kupitia Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa iliyofanyika tarehe 19 - 26 Januari 2026 Mkoani Tanga ambapo jumla ya wananchi 5,350 walipatiwa elimu ya fedha.

### 3.3.10 Usimamizi wa Mfumo wa Takwimu za Kitaifa

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kuendelea kutoa takwimu rasmi za kijamii, kiuchumi na mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Takwimu, SURA 351 na kufanya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi

Nchini. Hadi Aprili 2026, Wizara imeendelea kutoa kwa wakati takwimu rasmi za mwenendo wa uchumi ikiwemo Pato la Taifa - GDP, Fahirisi za Bei za Taifa za Mlaji - NCPI, Fahirisi za Bei za Mzalishaji - PPI, Fahirisi za Uzalishaji Viwandani - IIP, Fahirisi za Bei za Biashara - TPI na takwimu za mfumuko wa bei kwa kila mwezi, na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania. Aidha, ukusanyaji wa taarifa za shughuli/biashara za sekta isiyo rasmi umekamilika na ripoti ya matokeo muhimu itatolewa kwa wadau ifikapo Julai 2026.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya mapitio ya takwimu za Pato la Taifa kwa kuhuisha mwaka wa rejea kutoka 2015 kwenda 2019. Mapitio hayo yalilenga kukidhi matakwa ya kimataifa na

kujumuisha mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yaliyojitokeza katika kipindi hicho. Zoezi la kuhuisha mwaka wa kizio limefanyika sambamba na kuboresha takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya takwimu ikiwa ni pamoja na sensa, tafiti na taarifa za kiutawala.

**48.** ***Mheshimiwa Spika;*** uhuishaji wa takwimu za Pato la Taifa za mwaka wa kizio kutoka 2015 kwenda 2019 umebadilika muundo na ukubwa wa Pato la Taifa ambapo Pato la Taifa la mwaka 2019 kwa kutumia mwaka wa rejea wa 2019 limeongezeka kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na Pato la Taifa kwa mwaka wa rejea 2015. Mabadiliko mengine ni kuongezeka au kupungua kwa viwango vya ukuaji na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa na mabadiliko ya uwiano wa viashiria

mbalimbali. Aidha, matokeo ya kazi ya kuhuisha takwimu za Pato yamesababisha mabadiliko ya mwenendo wa Pato la Taifa pamoja na viashiria vingine vya kiuchumi.

### 3.3.11 Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Silaha za Maangamizi

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu (*Financial Action Task - FATF*); kufanya kaguzi kwa watoa taarifa na kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu sheria na kanuni zinazohusiana na utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi; kuboresha miundombinu ya TEHAMA na vitendea kazi vya Kitengo; na kushirikiana na kubadilishana uzoefu na mbinu mbalimbali na

wadau wa nje ya nchi katika udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu imefanya mapitio na kuhuisha Tathmini ya Taifa ya Vihatarishi ili kushughulikia masuala mapya yanayojitokeza na kuhakikisha inaendana kikamilifu na viwango vya FATF; na kuandaa na kusambaza Mwongozo maalum kwa wadau wote kuhusu utekelezaji wa sheria dhidi ya utakasishaji fedha haramu. Kazi nyingine zilizofanyika ni kutoa elimu kwa wadau 3,338 kuhusu wajibu wa kusimamia na kudhibiti utakasishaji fedha haramu; asasi 800 zilipatiwa mafunzo kuhusu ufadhili wa ugaidi na kuzingatia vihatarishi; kuboresha mfumo wa takwimu (NASMS) zinazohusiana na utakasishaji fedha haramu,

ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi na kuunganisha na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS); na kuratibu Mkutano wa Kimataifa wa Vitengo vya Kudhibiti Fedha Haramu Duniani (*EGMONT Group of FIUs*) uliofanyika Januari 26 - 30, 2026 Jijini Arusha.

### 3.3.12 Kusimamia Masuala ya Pamoja ya Fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Tume ya Pamoja ya Fedha ilipanga kufanya uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi ya Muungano kwa mwaka 2023/24 pamoja na bajeti ya mwaka 2024/25 na 2025/26 kwa shughuli za muungano, kufanya utafiti kuhusu ukopaji, uhudumiaji na ulipaji wa mikopo ya nje ya nchi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na kutoa elimu kwa wadau kuhusu uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, taarifa ya mwenendo wa mapato na matumizi ya Muungano ya mwaka 2023/24 na bajeti za mwaka 2024/25 na 2025/26 imekamilika. Aidha, taarifa ya stadi ya ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika ukopaji nje ya nchi na usimamizi wa madeni ya Serikali ya nje ya nchi imekamilika; na elimu kuhusu uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitolewa.

### 3.3.13 Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi za Wizara na Taasisi zake

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi pamoja na ukarabati wa majengo ya ofisi za Wizara na taasisi zake. Hadi Aprili 2026, ujenzi wa jengo la Ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika. Aidha, ujenzi wa nyumba ya makazi ya viongozi katika eneo la Mlimani, Uzunguni Dodoma umefikia asilimia 12.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, wizara ilipanga kuziwezesha baadhi ya taasisi zake kuboresha majengo ya ofisi na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Hadi Aprili 2026, jumla ya shilingi bilioni 6.02 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ambapo shilingi bilioni 4.49 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa

miundombinu ya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Kigoma na Zanzibar na ujenzi umefikia asilimia 98 na 45 mtawalia. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 1.53 kimetolewa kwa Soko la Bidhaa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi jijini Dar es Salaam, ambapo ujenzi umefikia asilimia 54.05.

### 3.3.14 Kusimamia Masuala ya Utafiti na Ubunifu

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ilianza kutekeleza Mwongozo wa Utafiti na Ubunifu kwa kutoa elimu kwa watumishi wote wa Wizara kuhusu ushiriki wao katika masuala ya utafiti na ubunifu. Aidha, Wizara ilipanga kupokea, kuchambua na kuidhinisha mawazo ya ubunifu yanayolenga kuboresha utoaji wa huduma, kujenga Mfumo wa

Kielektroniki wa Usimamizi wa Utafiti na Ubunifu, kufanya tathmini ya utoaji wa huduma kwa wadau na kufanya tafiti nne (4) za kisera. Hadi Aprili 2026, elimu kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Utafiti na Ubunifu ilitolewa kwa watumishi 483 wa Wizara, mawazo sita (6) ya ubunifu yalifanyiwa uchambuzi, na ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utafiti na Ubunifu umekamilika. Aidha, wizara ilifanya tafiti tano (5) za kisera ambazo ni Utafiti kuhusu Mfumo wa Ruzuku Zinazotolewa na Serikali; Ufanisi wa Mfumo wa Ugawaji wa Rasilimali wakati wa Kuweka Ukomo wa Bajeti na Kutoa Fedha kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Umma na Ofisi za Wakuu wa Mikoa; Mbinu ya Kutoza Ushuru kwa Faida ya Ziada katika Sekta ya Petroli; Tathmini ya athari za utekelezaji wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Kodi ya Mapato; na Tathmini ya Mwenendo wa

Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi katika Sekta ya Utalii ikihusisha TAWA, TANAPA na NCAA.

## 3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza baadhi ya majukumu kupitia taasisi zilizo chini yake ikiwemo taasisi za elimu; bodi za kitaalamu na kitaaluma; taasisi za benki na fedha; taasisi za usimamizi wa kodi; ununuzi na ugavi; michezo ya kubahatisha; taasisi za uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; na takwimu. Utekelezaji wa vipaumbele vya taasisi ni kama ifuatavyo:

### 3.4.1 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kuendelea kuboresha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato ya Serikali ikiwemo TANCIS na IDRAS, pamoja na kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa umma ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kupunguza upotevu wa mapato unaotokana na udanganyifu wa taarifa za miamala na biashara za magendo. Hadi Aprili 2026, Mamlaka imekamilisha maboresho ya mifumo ya IDRAS na TANCIS na kuanza kutumika. Aidha, Mamlaka imeendelea kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kupunguza upotevu wa mapato kupitia vipindi 289 vya redio, 38 vya televisheni, programu 104 za uhamasishaji, machapisho 13,500,

maonesho 21, video 298 na *infographics* 210, pamoja na warsha 56 na kampeni ya “Dai Risiti Yako” iliyofikia walipakodi 1,563,996.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizo za kiutawala na maboresho ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato zimewezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya jumla ya mapato ghafi ya shilingi trilioni 30.25, sawa na ufanisi wa asilimia 105 ya lengo la kipindi cha rejea. Kati ya kiasi hicho, mapato ya forodha yalikuwa shilingi trilioni 11.49, kodi ya mapato shilingi trilioni 10.95, kodi ya mlaji shilingi trilioni 6.32, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 1.22 na kodi nyingine shilingi bilioni 266.72.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Rufani za Kodi ilipanga kuendelea

kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kuandaa Juzuu ya Taarifa za Sheria za Kodi Tanzania, na kuhuisha Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408 pamoja na kanuni zake. Hadi Aprili 2026, jumla ya mashauri ya kodi 1,193 (rufaa 1,078 na maombi 115) ya kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi trilioni 1.68 na dola za Marekani 11,183,803.03, sawa na shilingi bilioni 29.33 yamesajiliwa. Aidha, mashauri ya maombi 778 (rufaa 698 na maombi 80) yenye kiasi cha kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi trilioni 4.84 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Baraza la Rufani za Kodi lilipanga kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi

300 yanayotokana na maamuzi ya Bodi ya Rufani za Kodi. Aidha, hadi Juni 30, 2025, Baraza lilikuwa na mashauri 217 (Rufaa 206 na maombi 11) yenye kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi trilioni 5.51. Katika kipindi cha Julai 1, 2025 hadi Aprili 30, 2026, Baraza limesajili mashauri 201 (rufaa 134 na maombi 67) yenye kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi bilioni 890.25. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya mashauri 205 (rufaa 162 na maombi 43) yenye kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi bilioni 734.14 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi. Mashauri 34 (rufaa 33 na ombi 1) yenye kodi zinazobishaniwa zenye thamani ya shilingi trilioni 2.44 yamesikilizwa na yapo kwenye hatua ya kutolewa uamuzi.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa

za Kodi ilipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya taasisi; kupokea na kutatua malalamiko ya walipakodi; kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kupokea na kuchakata malalamiko na taarifa za kodi; kuratibu mchakato wa kutunga sheria mpya ya Taasisi; na kujenga uwezo kwa watumishi katika maeneo ya uendeshaji na usuluhishi wa malalamiko. Hadi Aprili 2026, elimu kwa umma imetolewa katika Maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki ambapo wananchi 35,462 walipatiwa elimu. Aidha, jumla ya malalamiko na taarifa 176 zilipokelewa, ambapo jumla ya malalamiko na taarifa 34 zimefanyiwa kazi na malalamiko na taarifa 142 zipo katika hatua mbalimbali za usikilizaji. Vilevile, ujenzi wa Mfumo wa Kupokea Malalamiko na Taarifa za Kodi kwa njia ya simu janja umekamilika na mfumo wa

kuwasilisha malalamiko na taarifa za kodi kwa njia ya simu umefikia hatua ya majaribio. Kadhalika, watumishi 10 wamepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya utatuzi mbadala wa malalamiko na taarifa za kodi.

#### 3.4.2 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kutekeleza yafuatayo: Kuhakikisha mfumuko wa bei unaendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3 hadi 5, ukwasi katika soko unaendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi; kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za kigeni; na kuboresha mifumo ya malipo ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu nchini.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, utekelezaji wa sera ya fedha uliimarishwa na kuhakikisha ukwasi wa kutosha katika soko la fedha baina ya benki, sambamba na mahitaji ya shughuli za uchumi. Kiwango cha ukwasi kiliongezeka, na hivyo kuimarisha uwezo wa benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi, na kuchangia ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 20.2 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki ilibaki ndani ya wigo wa asilimia ±2 wa kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR). Mwenendo huu unaashiria uwezo wa Benki Kuu katika kudhibiti viwango vya riba vya muda mfupi, ili kufikia malengo ya mfumuko wa bei na kusaidia ukuaji wa uchumi.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki Kuu imeendelea kutekeleza mpango wa kuimarisha akiba ya dhahabu ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya tani 17.64 za dhahabu zimenunuliwa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2,616.77 hivyo, akiba ya dhahabu imefikia tani 24.21 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,591.39 tangu kuanzishwa kwa mpango huo. Aidha, Benki imezindua Mfumo Mkuu Jumuishi wa Benki (*Integrated Central Banking System*) kwa lengo la kurahisisha uhamishaji wa fedha na kuongeza ufanisi katika huduma za malipo ya Serikali.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu, Benki iliboresha mfumo wa TIPS kuwezesha uhamishaji wa fedha kutoka nje ya nchi na kuunganishwa na

mfumo wa Serikali wa ankara za malipo (GePG); kuchochea matumizi ya msimbo wa malipo wa Taifa (TANQR) ambapo idadi ya watoa huduma waliosajiliwa iliongezeka kutoka 23 Juni 2025 hadi 27 ikiwemo benki 21 na watoa huduma za fedha mtandao sita (6); na kutoa leseni kwa watoa huduma wa mifumo ya malipo wasio taasisi za kibenki 77.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Bima ya Amana ilipanga kushughulikia amana za wateja wa iliyokuwa Benki ya FBME; kuboresha Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Utendaji Kazi na Rasilimali za Taasisi; kukusanya maoni ya wadau kuhusu utungaji wa Sheria ya Kinga ya Amana; kutoa elimu kwa umma kuhusu Mfumo wa Bima ya Amana; kukusanya mikopo chechefu ya wakopaji wa benki zilizo chini ya ufilisi; na kuandaa

miongozo ya usimamizi wa fedha za Mfuko wa Bima ya Amana.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwishoni mwa Aprili 2026, Bodi ilifanikiwa kulipa gawio la ziada la ufilisi la asilimia 30 kwa wadai wa amana wa Benki ya FBME, sawa na gawio la ufilisi la asilimia 55; kuboresha Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Utendaji Kazi na Rasilimali za Taasisi; kukamilisha ukusanyaji wa maoni kuhusu rasimu ya Sheria ya Kinga ya Amana; kutoa mafunzo kwa makundi maalumu kupitia maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; kukusanya mikopo chechefu ya shilingi bilioni 96.27, sawa na asilimia 46.6 kutoka kwa wakopaji wa benki zilizo chini ya ufilisi; na kukamilisha uandaaji wa miongozo ya usimamizi wa fedha za Mfuko wa Bima ya

Amana ikiwemo waraka kuhusu njia mbadala za uwekezaji wa fedha za Mfuko wa Bima ya Amana, Sera na Mwongozo wa Uwekezaji wa Mfuko wa Bima ya Amana na waraka wa kuweka kinga kwenye amana za akaunti za kampuni za simu za mkononi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 69.53; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 30.65 kutoka shilingi bilioni 24.68 mwaka 2024; kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 300 ikilinganishwa na shilingi bilioni 286.38 mwaka 2024; kuongeza thamani ya mali kufikia shilingi trilioni 1.13 kutoka shilingi bilioni 917.41 mwaka 2024; na kufuatilia marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 120.00.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Desemba 2025, TADB ilifanikiwa kutoa mikopo ya jumla ya shilingi billioni 429.74, sawa na asilimia 127.9 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, sekta ndogo ya ununuzi wa mazao iliongoza kwa kupokea mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 209.23, sawa na asilimia 48.7, ujenzi wa viwanda na uchakataji mazao shilingi bilioni 127.04, sawa asilimia 29.6, na makundi maalum ya wanawake na vijana shilingi bilioni 53.46, sawa na asilimia 12.4. Aidha, TADB ilifanikiwa kutengeneza faida kabla ya kodi ya shillingi bilioni 35.35, sawa na asilimia 115 ya lengo la mwaka, na thamani ya mali za Benki imefikia shillingi trilioni 1.31, sawa na asilimia 115 ya lengo la mwaka. Vilevile, TADB ilifanikiwa kufuatilia na kukusanya marejesho ya mikopo ya jumla ya shilingi billioni 260.2, sawa na asilimia 216.83 ya lengo.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Maendeleo (TIB) ilipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 20; kuongeza mali hadi shilingi bilioni 478 kutoka shilingi bilioni 453 mwaka 2024; na kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya shilingi bilioni 11.14 na mikopo iliyo ndani ya mizania ya shilingi bilioni 25.03. Hadi Desemba 2025, TIB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 8.23, sawa na asilimia 41.15 ya lengo na thamani ya mali ilifikia shilingi bilioni 486, sawa na asilimia 101.67 ya lengo. Aidha, TIB ilikusanya shilingi bilioni 1.86, sawa na ailimia 16.70 ya lengo kutoka kwenye mikopo iliyo nje ya mizania na shilingi bilioni 9.25 kutoka kwenye mikopo iliyo ndani ya mizania, sawa na asilimia 36.96 ya lengo.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Biashara Tanzania (TCB) ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 316.36; kukuza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 65.02; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,483.07; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,858.26; kukuza mali za hadi shilingi bilioni 2,274.44 kutoka shilingi bilioni 1,741.85 mwaka 2024; kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 192.96 kutoka shilingi bilioni 150.85 mwaka 2024; na kuongeza idadi ya wateja hadi 1,214,059 kutoka wateja 914,059 mwaka 2024.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2025, TCB ilizalisha mapato ya shilingi bilioni 287.41, sawa na asilimia 90.85 ya lengo; kutengeneza faida kabla ya kodi shilingi bilioni 47.59, sawa na asilimia 73.20 ya lengo; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,494.56, sawa na asilimia

100.77 ya lengo. Kati ya kiasi cha mikopo iliyotolewa, asilimia 49.3 ilielekezwa kwa watu binafsi; biashara asilimia 13.8; usafiri, usafirishaji na mawasiliano asilimia 6.8; kilimo asilimia 3; na asilimia 27.1 imeelekezwa kwenye sekta nyingine. Aidha, TCB ilikusanya amana za shilingi bilioni 1,663.19, sawa na asilimia 89.5 ya lengo; kuongeza thamani ya mali kufikia shilingi bilioni 2,277.88 kutoka shilingi bilioni 1,741.85 mwaka 2024; kukuza mtaji kwa shilingi bilioni 28.19 hadi shilingi bilioni 179.04 kutoka shilingi bilioni 150.85 mwaka 2024; na kuongeza idadi ya wateja kutoka 914,059 hadi 1,030,977 mwaka 2024, sawa na ongezeko la wateja 116,918.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF ulipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 48

ikilinganishwa na shilingi bilioni 45.2 mwaka 2024; kukuza faida kabla ya kodi shilingi bilioni 1.14 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.09 mwaka 2024; kukuza mtaji kutoka shilingi bilioni 58.99 mwaka 2024 hadi shilingi bilioni 61.0; kuongeza idadi ya wateja kutoka wateja 55,743 mwaka 2024 hadi wateja 60,000; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya Mfuko kutoka shilingi bilioni 1.49 mwaka 2024 hadi shilingi bilioni 2.0 na kuongeza marejesho ya mikopo iliyo ndani ya mizania kutoka shilingi bilioni 41.63 mwaka 2024 hadi shilingi bilioni 53.05; na kuzalisha mapato ya jumla ya shilingi bilioni 12.13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.32 mwaka 2024.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2025, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 43.26 kwa wajasiriamali wadogo 38,545, sawa na asilimia 90.13 ya lengo. Sekta

zilizonufaika na mikopo hiyo ni kilimo shilingi bilioni 1.90, biashara bilioni 9.43, huduma za fedha shilingi bilioni 22.40, ujenzi shilingi bilioni 0.87 na mikopo binafsi kwa matumizi ya kawaida (Consumer Loans) shilingi bilioni 8.66. Aidha, Mfuko ulitengeneza faida ya shilingi bilioni 2.29, sawa na asilimia 200.88 ya lengo; mtaji ulifikia shilingi bilioni 59.93 ikilinganishwa na matarajio ya kufikia shilingi bilioni 61.0, sawa na ufanisi wa asilimia 98.25; wajasiriamali wadogo walifikia 38,545, sawa na asilimia 101 ya lengo; kukusanya shilingi bilioni 1.49, sawa na asilimia 74.50 ya lengo la marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya Mfuko; kukusanya shilingi bilioni 41.63, sawa na asilimia 95.93 ya lengo la mikopo iliyo katika mizania ya Mfuko; na kukusanya mapato ya shilingi bilioni 9.71, sawa na ufanisi wa asilimia 80 ya lengo la mwaka.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko hadi shilingi bilioni 4,085.88 kutoka shilingi bilioni 3,268.70 mwaka 2024/25; kuongeza idadi ya wawekezaji hadi 520,370 kutoka 473,063 mwaka 2024/25; na kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 37.40 kutoka shilingi bilioni 32.85 mwaka 2024/25. Hadi Aprili 2026, rasilimali za mifuko ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 4,741.90, sawa na ufanisi wa asilimia 116.06 ya lengo; idadi ya wawekezaji iliongezeka kutoka 473,063 hadi 621,893, sawa na asilimia 131.46 ya lengo; na faida kabla ya kodi ilifikia shilingi bilioni 46.63, sawa na asilimia 124.68 ya lengo la mwaka.

### 3.4.3 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**76. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imepanga kujenga moduli mbili (2) ambazo ni Moduli ya Minada ya Ununuzi na Moduli ya Katalogia ya Bidhaa na Huduma; kufanya kaguzi za ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na kaguzi za thamani halisi ya fedha kwa taasisi 570; na kujenga uwezo kwa wadau 2,000 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya Mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410.

**77. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Mamlaka imekamilisha kazi ya ujenzi wa Moduli ya Minada ya Kielektroniki (*e-Auction Module*) na Moduli ya Orodha ya Bidhaa na Huduma kwa njia ya Kielektroniki (*e-Catalogue*) na kuanza kutumika. Aidha, Mamlaka imefanya

ukaguzi wa uzingatiaji wa kanuni na taratibu za ununuzi katika taasisi nunuzi 833, ukaguzi wa thamani halisi ya fedha katika taasisi nunuzi 152 na ukaguzi wa uzingatiaji wa kanuni na taratibu za ununuzi katika taasisi nunuzi 645 katika ngazi za chini za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, Mamlaka imejenga uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kwa jumla ya wadau 10,678 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ilipanga kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi 200; kusajili wataalamu 3,000 wa ununuzi na ugavi; kudahili na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000; kuendesha mafunzo na

ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 5,000 wa ununuzi na ugavi; na kufanya maboresho ya Mfumo wa Usajili wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Mtandaoni Toleo la II (ORS).

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi umefanyika katika taasisi 98, sawa na asilimia 49 ya lengo la mwaka; wataalam 2,544 wa ununuzi na ugavi wamesajiliwa, sawa na asilimia 84.8 ya lengo; watahiniwa 1,463 wameshiriki katika mitihani ya kitaalamu, sawa na asilimia 73.2 ya lengo; mafunzo kuhusu ununuzi na ugavi yamefanyika kwa wataalamu 1,125, sawa na asilimia 22.5 ya lengo; na maboresho ya Mfumo wa Usajili wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Mtandaoni Toleo la II (ORS) yapo katika hatua ya ukusanyaji wa mahitaji.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma ilipanga kusajili na kushughulikia rufaa 55 na maombi matano (5); kuandaa Mpango Mkakati wa Mamlaka wa 2026/27 – 2030/31; kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia mfumo wa NeST kwa wazabuni 1,680 na wakuu wa idara na vitengo vya ununuzi, TEHAMA na sheria wapatao 1,500; na kuboresha moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko kupitia mfumo wa NeST.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, rufaa 35 zilisajiliwa, sawa na asilimia 63.6 pamoja na maombi mawili (2), sawa na asilimia 40 ambapo rufaa 28 na maombi mawili (2) yamesikilizwa na kutolewa uamuzi. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilisikiliza na kutoa

uamuzi katika rufaa tano (5) zilizobaki kutoka mwaka 2024/25. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2026/27–2030/31); kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia mfumo wa NeST kwa wazabuni 1,296 pamoja na watumishi wa taasisi za umma 705 kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe na Iringa; na moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko kupitia mfumo wa NeST imeboreshwa.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini ulipanga kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam; kuwezesha upatikanaji wa ithibati ya kimataifa katika utoaji wa huduma (ISO Certified); kufanya upembuzi yakinifu wa

mradi wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari kwa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma; kuwezesha ufungamanishwaji wa Mfumo wa Kiutendaji wa Wakala (GIMIS) na mifumo mingine ya Serikali ya MUSE na GAMIS; na kukamilisha ujenzi wa ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara) na Korogwe (Tanga).

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam upo hatua ya usanifu; wakala umekamilisha mafunzo kwa watumishi wote na uandaaji wa nyaraka (SOPs) za kupata ithibati ya ubora (ISO Certified); magari manne (4) ya kubeba mafuta yamenunuliwa na kupokelewa; upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi (CNG) pamoja na umeme kwa magari

katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma upo hatua ya ununuzi wa mshauri elekezi; ufungamanishaji wa moduli zinazohusu ununuzi wa vifaa vya ofisi, mafuta na vyombo vya moto katika mifumo ya GIMIS na NeST umekamilika, na ujenzi wa ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika wilaya za Korogwe umefikia asilimia 65, Mbarali asilimia 40, na Masasi asilimia 75.

### 3.4.4 Usimamizi wa Bima Tanzania

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) Tanzania ilipanga kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Shughuli za Bima Mtawanyo; kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kusomana na mifumo mingine ya taasisi za Serikali; kufanya ukaguzi wa wadau

wa bima 168 (kampuni za bima 20 na matawi 22), madalali 20, mawakala 80, wakala wa kibenki 10, matawi ya wakala wa kibenki 8, na watoa huduma za bima kidijiti watano (5) na washauri bima mtawanyo watatu (3); kufanya mapitio ya Sheria ya Bima Sura 394; na kusajili na kutoa leseni mpya 100 za huduma za bima.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Mamlaka imekamilisha kazi ya ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi (*Insurance Regulatory Integrated System - IRIS*); kufanya maboresho ya Mfumo wa TIRA MIS na kuunganisha na mifumo ya taasisi za Serikali na sekta binafsi ikiwemo Wizara ya Afya, TRA, ZRA, LATRA, kampuni za bima, EWURA, Benki Kuu pamoja na benki ya NMB; kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo kwa wasajiliwa wa huduma za bima 168 ikiwemo

kampuni za bima 20 na matawi yake 22, madalali/washauri wa bima 20, mawakala wa bima 80, benki wakala 10 na matawi yake manane (8), watoa huduma za bima kidijiti watano (5) na washauri wa bima mtawanyo watatu (3); kukusanya maoni ya wadau kuhusu marekebisho ya Sheria ya Bima Sura 394; na kusajili na kutoa leseni mpya 230 kwa watoa huduma za bima.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kuongeza faida ghafi hadi shilingi bilioni 90.58 kutoka shilingi bilioni 85.56 mwaka 2024/25; kufanya mapitio ya bidhaa nane (8) za bima za mali na ajali pamoja na bidhaa tatu (3) za bima za maisha; na kuboresha vituo viwili (2) vya kuhifadhi data na urejeshaji huduma baada ya majanga. Hadi Aprili 2026, Shirika limetengeneza faida ghafi ya

shilingi bilioni 31.28, sawa na asilimia 34.5 ya lengo; bidhaa mbili (2) za bima za mali na ajali zimefanyiwa maboresho ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za bima za moto na bima za nyumba za makazi; bidhaa tatu (3) za bima ya maisha, bima ya malengo, bima za vikundi na bima ya mazishi zimefanyiwa maboresho ili kukidhi mahitaji ya sasa ya soko. Vilevile, Shirika limeboresha kituo okozi cha majanga.

### 3.4.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Bidhaa

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji kwa watu milioni 15; kuongeza watendaji na wataalamu wa masoko ya mitaji kwa asilimia 10 ili kufikia 993;

na kushirikiana na wadau wa masoko ya mitaji katika kubuni na kuanzisha bidhaa mpya sita (6). Hadi Aprili 2026, Mamlaka ilifanikiwa kuidhinisha bidhaa mpya 18 sawa na asilimia 300 ya lengo na kuwezesha taasisi na kampuni katika sekta ya umma na sekta binafsi kupata fedha za kugharamia biashara na miradi ya maendeleo; kutoa elimu kwa watu zaidi ya milioni 17 kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano ya kitaifa na kimataifa na maonesho mbalimbali kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji, sawa na asilimia 113.33 ya lengo. Aidha, Mamlaka imeongeza watendaji na wataalamu wa masoko ya mitaji kwa asilimia 10.5 na kufikia 1,139.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na mfumo mzima wa

uuzaji wa bidhaa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania; na kufanya mauzo ya bidhaa 11 ikiwemo ufuta, dengu, choroko, mbaazi, soya, kakao, madini, kahawa, korosho, chai na mifugo. Hadi Aprili 2026, elimu imetolewa kupitia kampeni za uhamasishaji wa matumizi ya Soko la Bidhaa kwa wadau 3,329 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Arusha, Lindi, Songwe, Ruvuma, Mtwara na Morogoro. Aidha, jumla ya bidhaa 10, sawa na asilimia 90.9 zimeuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania ambazo ni kakao, chai, madini ya vito, korosho, ufuta, kahawa, dengu, mbaazi, maharage ya soya na choroko.

### 3.4.6 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara ya Fedha zimeendelea

kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa shauri elekezi kuhusu masuala mbalimbali ya fedha, mipango na takwimu.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kilipanga kudahili wanafunzi 18,400 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 40 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti 28; na kutoa huduma elekezi 12. Hadi Aprili 2026, Chuo kilifanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 18,552 katika ngazi na fani mbalimbali, sawa na asilimia 100.08 ya lengo. Aidha, Chuo kinaendelea kusomesha jumla ya watumishi 46 ikiwemo 25 katika ngazi ya uzamili na 21 katika ngazi ya uzamivu. Vilevile, Chuo kimefanya tafiti 41 na kutoa huduma elekezi moja (1).

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 15,556 katika ngazi ya astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili; kuendeleza watumishi 10 katika shahada ya uzamili na 29 katika shahada ya uzamivu; kufanya tafiti 10; na kutoa huduma elekezi sita (6). Aidha, Chuo kilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo kujenga jengo la taaluma katika eneo la Miyuji Kampasi Kuu Dodoma na jengo la bweni awamu ya pili Kampasi ya Mwanza. Hadi Aprili 2026, jumla ya wanafunzi 15,805 wamedahiliwa katika Kampasi Kuu Dodoma na Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa Mwanza sawa na asilimia 101.60 na watumishi 69 wanaendelea na masomo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi ikiwemo watumishi 45 katika Shahada ya Uzamivu na 14 Shahada ya

Uzamili. Aidha, ujenzi wa jengo la taaluma katika eneo la Miyuji Dodoma umefikia asilimia 75 na ujenzi wa jengo la bweni awamu ya pili Kampasi ya Mwanza umefikia asilimia 45. Vilevile, Chuo kimefanikiwa kutoa huduma elekezi mbili (2).

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Chuo cha Uhasibu Arusha kilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 27,420 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 129 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti tano (5); kutoa huduma elekezi nne (4); na kuendelea na ujenzi wa jengo la uhasibu na fedha pamoja na bweni kampasi ya Dodoma. Hadi Aprili 2026, Chuo kimefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 20,727 katika ngazi na fani mbalimbali, sawa na asilimia 76 ya lengo; kuendeleza watumishi 114

katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; na kufanya tafiti tatu (3). Aidha, ujenzi wa jengo la uhasibu na fedha pamoja na bweni umefikia asilimia 10 na asilimia 5 mtawalia.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilipanga kudahili jumla ya wanafunzi 33,581 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 111 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti 10; kutoa huduma elekezi tano (5); na kuendelea na ujenzi wa majengo ya taaluma katika kampasi ya Kigoma na Zanzibar. Hadi Aprili 2026, jumla ya wanafunzi 35,847 wamedahiliwa, sawa na asilimia 106.70 ya lengo, watumishi 46 wamejengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya uzamivu na uzamili, Taasisi imefanya tafiti sita (6) na kutoa huduma

elekezi tisa (9) katika maeneo mbalimbali. Aidha, ujenzi wa majengo ya taaluma katika kampasi ya Kigoma na Zanzibar umefikia asilimia 98 na 25 mtawalia.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kilipanga kudahili wanafunzi 3,000 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 29 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti tano (5); na kutoa huduma elekezi nne (4). Hadi Aprili 2026, Chuo kimefanikiwa kudahili wanafunzi 2,152 katika ngazi na fani mbalimbali, sawa na asilimia 71.7 ya lengo, kuendeleza watumishi 28 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti nane (8); na kutoa huduma elekezi nne (4).

### 3.4.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kuendelea na Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2025; kukamilisha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; kufanya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2024/25; na kukamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi katika mkoa wa Pemba, Lindi na Simiyu. Hadi Aprili 2026, Ofisi imefanya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2025; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; na Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2024/25. Taarifa za matokeo ya kina ya tafiti hizi zinatarajiwa kusambazwa mwezi Juni 2026. Aidha, ujenzi wa majengo ya ofisi katika mkoa wa Pemba

umefikia asilimia 55, Lindi asilimia 6 na Simiyu asilimia 23.

### 3.4.8 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilipanga kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 14,500; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa watahiniwa 15,120; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa

wahitimu 1,950 wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa watahiniwa; kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 150; kutoa ushauri wa kiufundi katika matumizi ya viwango vya uhasibu na ukaguzi katika uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa kampuni nane (8) na kukamilisha uundaji wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji, utambuzi na uhakiki wa taarifa za fedha zilizokaguliwa nchini kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuzalisha taarifa za fedha zaidi ya moja kwa taasisi/kampuni ili kukwepa kodi.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Bodi imesajili wahasibu na wakaguzi 314 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kufanya mafunzo ya kitaaluma ya uandaaji na ukaguzi

wa hesabu kwa wahasibu na wakaguzi 14,650; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 65; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 49 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa awamu ya kwanza kwa watahiniwa 8,120; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa awamu ya pili kwa watahiniwa 1,365; kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 169; na kutoa ushauri wa kiufundi katika matumizi ya viwango vya uhasibu na ukaguzi katika uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa kampuni saba (7). Aidha, Mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji, utambuzi na uhakiki wa taarifa za fedha

zilizokaguliwa (NBAA Verification Number) umekamilika na umeanza kutumika.

### 3.4.9 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ilipanga kutoa leseni 14,124 ikijumuisha leseni mpya 845 na kuhuisha leseni 13,279; kufanya kaguzi 12 kwa kuzingatia vihatarishi (*risk based*) katika michezo ya kubahatisha; kutekeleza operesheni nne (4) za kudhibiti michezo haramu ya kubahatisha; kukusanya jumla ya mapato ya shilingi bilioni 29.89; kuendelea kuelimisha jamii kuhusu athari hasi za michezo ya kubahatisha na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Bodi imetoa leseni 7,747, sawa na asilimia 54.85 ya lengo ikijumuisha leseni mpya 1,813 na zilizohuishwa 5,934; kufanya kaguzi tisa (9) katika michezo ya Kasino, Kubashiri Matokeo na Mashine za Dubwi (*Slot Machines*), sawa na asilimia 75 ya lengo; na kufanya operesheni tatu (3) za kudhibiti michezo haramu ya kubahatisha, sawa na asilimia 75 ya lengo. Aidha, Bodi imekusanya jumla ya shilingi bilioni 18.76, sawa na asilimia 62.75 ya lengo la mwaka na kufanya programu tatu (3) za kuelimisha jamii juu ya michezo ya kubahatisha na dhana nzima ya kucheza kwa kiasi (*responsible gaming*), ambazo ni “Elimika na GBT”, “Mkeka Unachana”, na “Wakati Wao Bado”.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi imeendelea kusimamia mchezo wa Bahati Nasibu ya Taifa uliozinduliwa rasmi Aprili 2025 ili kuhakikisha unaendeshwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na kuleta tija kwa maendeleo ya kijamii na uchumi. Hadi Aprili 2026, mchezo huu umezalisha ajira 484 ambapo kati ya hizo, ajira 29 ni za moja kwa moja na 455 zisizo za moja kwa moja kupitia uwakala. Aidha, jumla ya shilingi 72,063,555.77 zimekusanywa zikijumuisha: kodi ya michezo ya kubahatisha (Gaming Tax) shilingi 10,328,944.77, kodi ya washindi (Tax on Winnings) shilingi 59,152,375.00 na tozo (Gaming Levy) shilingi 2,582,236.00.

## 3.5 MCHANGO WA TAASISI KATIKA MFUKO MKUU WA HAZINA YA SERIKALI

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, taasisi zilizo chini ya wizara zilikadiriwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 427.17. Kati ya kiasi hicho, gawio ni shilingi bilioni 388.40, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 22.92 na michango mingine ikijumuisha ziada ya mtaji shilingi bilioni 15.85. Hadi Aprili 2026, taasisi zimefanikiwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 341.53, sawa na asilimia 79.95 ya lengo la mwaka, ambapo shilingi bilioni 322.38 zimetokana na gawio sawa na ufanisi wa asilimia 83.00, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi, shilingi bilioni 13.49, sawa na

ufanisi wa asilimia 59.00 na michango mingine ikijumuisha ziada shillingi bilioni 5.66, sawa na ufanisi wa asilimia 36.00.

## 3.6 MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA FUNGU 045 - OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA 2025/26

**102.** ***Mheshimiwa spika,*** kwa mwaka 2025/26, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, ukaguzi wa ufanisi na kiufundi ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma; kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukaguzi wa hesabu za fedha, ufanisi, kiufundi na thamani halisi ya fedha; kuzijengea

uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha za Umma na kamati za kisekta kuhusu mamlaka na majukumu ya CAG, uchambuzi wa ripoti za ukaguzi pamoja na kutambua mbinu za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo; na kujenga uwezo wa wakaguzi juu ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA inayotumika katika ukusanyaji wa mapato na matumizi, ukaguzi wa wakati halisi (*real-time audit*), ukaguzi wa ufanisi na kiufundi, ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na mabadiliko ya viwango vya ukaguzi vya kimataifa.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2026, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: kuwasilisha katika Bunge jumla ya ripoti jumuifu 6 za ukaguzi wa

mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/25 (Serikali Kuu, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Miradi ya Maendeleo, Mashirika ya Umma, Ufanisi na Mifumo ya Tehama); kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha (LAAC, PAC, PIC na PBC) na Makatibu wa Kamati hizo kuhusu uelewa wa Mamlaka, Majukumu na Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG); na kuendelea na ujenzi wa Mfumo wa Uvunaji wa Taarifa za Fedha (ADLS) awamu ya tatu kwa ajili ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali.

## 4.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA NA HATUA ZA KUKABILIANA NAZO

### 4.1 Changamoto

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya wizara, changamoto mbalimbali zilijitokeza ikiwemo:

i. Kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha ya nje na hivyo kuathiri upatikanaji wa kiwango cha mikopo iliyotarajiwa;

ii. Mwitikio mdogo wa matumizi ya teknolojia na mifumo ya kielektroniki ya malipo na hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi;

iii. Kuongezeka kwa migogoro ya kibiashara na kivita duniani kulikoathiri mnyororo wa

biashara na kuongeza gharama za kupata bidhaa na huduma mbalimbali;

iv. Kubadilika kwa sera za washirika wa maendeleo na kusababisha kupungua kwa misaada katika maoteo ya mwaka 2026/27;

v. Kiwango kikubwa cha malimbikizo ya madeni na madai ya wakandarasi, watoa huduma na wazabuni; na

vi. Kuongezeka kwa mahitaji ya kujenga uwezo kwa watumishi wa umma kuhusu uzingatiaji wa masuala ya mazingira na matumizi ya Akili Unde (AI) katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

## 4.2 Mikakati

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imeendelea

kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo:

i. Kuimarisha mifumo na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

ii. Kuongeza kiwango cha ukopaji kutoka soko la ndani la fedha kufuatia mwenendo mzuri wa minada ya hatifungani za serikali na kampuni;

iii. Kuhamasisha na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika malipo, utoaji huduma, ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma;

iv. Kuboresha mazingira ya uwekezaji, biashara na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani;

v. Kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni na madai ya wakandarasi, watoa huduma na

wazabuni; na

vi. Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga uwezo kwa watumishi kuhusu uzingatiaji wa masuala ya mazingira na matumizi ya Akili Unde (AI) katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

## 5.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/27

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya wizara, taasisi zake na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26, sasa kwa heshima na unyenyekevu naomba kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2026/27 kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2026/27 umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na Dira 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29); Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Mikakati na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe na mazingira.

**108.** ***Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na kuzingatia miongozo hiyo, Wizara ya Fedha inatambua kuwa kuna vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti. Vihatarishi hivyo ni kama viliyoainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29). Hivyo, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na vihatarishi hivyo ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa mipango yake.

## 5.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2026/27

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Wizara ya Fedha inatarajia kutekeleza vipaumbele vinane (8) ambavyo ni:

i. Kusimamia kwa weledi uchumi jumla ili kufikia ukuaji wa asilimia 6.3 mwaka 2026, mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 na akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4);

ii. Kuimarisha nidhamu ya usimamizi wa fedha serikalini (**fiscal discipline**) kwa kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato, ugawaji wa rasilimali, ununuzi na thamani halisi ya fedha na kupunguza kadiri itakavyowezekana uhamisho wa bajeti baina ya mafungu (**reallocation between votes**);

iii. Kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato, misaada na mikopo ili kufikia lengo la kuchangia **shilingi bilioni 55,200.75** katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, sawa asilimia 88.6 ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya jumla ya **shilingi bilioni 62,334.19**;

iv. Kulipa kwa wakati riba na mtaji wa deni la Serikali linalotarajiwa kuiva, lenye thamani ya **shilingi bilioni 15,102.80** ili kukidhi matakwa ya kimikataba na kuendelea kujenga na kuimarisha imani ya Serikali katika masoko ya fedha ya kikanda na kimataifa;

v. Kutenga na kutoa **shilingi bilioni 100.00** kila mwezi kwa ajili ya malipo ya

madeni ya watumishi, wakandarasi, watoa huduma na wazabuni;

vi. Kuboresha mfumo wa ugawaji wa rasilimali fedha kwa kuzingatia matokeo ya tafiti za kitaalamu ili kuondoa urudufu na kuimarisha uwiano wa mgawanyo wa rasilimali fedha katika mpango na bajeti ya Serikali, kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na miongoni mwa Serikali za Mitaa;

vii. Kufanya tathmini ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali kwa Kuzingatia Mfumo wa Programu (Programme Based Budgeting – PBB) kwa lengo la kuwezesha maamuzi ya mabadiliko ya mfumo wa usimamizi wa mpango na bajeti ya Serikali; na

viii. Kujenga uwezo wa watumishi kuhusu uzingatiaji wa masuala ya Mazingira, Jamii na Utawala Bora pamoja na matumizi ya Akili Unde (AI) katika usimamizi wa fedha za umma na uchumi.

## 5.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2026/27

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, ukaguzi wa ufanisi, ukaguzi wa kiufundi, ukaguzi wa mifumo, ukaguzi wa kiuchunguzi pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kuwajengea uwezo watumishi katika maeneo

ya ukaguzi na utendaji; kuendelea na ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Ruvuma, Mwanza na Tanga na ukarabati wa jengo la ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Ukaguzi (National Audit Academy).

## 5.3 Mpango wa Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2026/27

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpango wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2026/27 ni kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekadiriwa kukusanya mapato ghafi ya kodi na

yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 41,009.60. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 39,641.42 ni mapato ya kodi na shilingi bilioni 1,368.18 ni mapato yasiyo ya kodi. Aidha, TRA itaendelea kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kutoa elimu ya kodi kupitia kampeni mbalimbali, kuimarisha mazingira rafiki ya ulipaji kodi na kudhibiti ukwepaji kodi na vitendo vya rushwa kwa kutumia uchunguzi wa kisasa na mbinu za ukaguzi zinazotegemea taarifa za kiintelijensia.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Bodi ya Rufani za Kodi imepanga kuendelea kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na malalamiko dhidi ya maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kuandaa Juzuu ya Taarifa za Sheria za Kodi

Tanzania na kuhuisha Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408 pamoja na kanuni zake. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi linatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi 360 yanayotokana na maamuzi ya Bodi ya Rufani za Kodi.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imepanga kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya *Tax Ombudsman*, kuunganisha mfumo wa malalamiko na mifumo ya TRA, kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu na shughuli za taasisi na kupokea na kusuluhisha malalamiko ya walipakodi.

### 5.3.2 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya kiwango cha asilimia 3–5 na kuimarisha uthabiti wa uchumi. Benki itaongeza na kuboresha vyanzo vya akiba ya fedha za kigeni ili kudumisha uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne, kuimarisha masoko ya fedha ya ndani, na kuimarisha mifumo ya usimamizi na udhibiti wa sekta ya fedha kwa kuzingatia viwango vya kikanda na kimataifa. Aidha, Benki itaimarisha ulinzi wa watumiaji wa huduma za fedha, kukuza elimu ya fedha, kuimarisha usalama wa

kimtandao na uimara wa miundombinu ya kifedha, kutumia teknolojia za kidijitali na akili unde kuongeza ufanisi na ubora wa huduma, kuimarisha usimamizi wa takwimu, na kuimarisha huduma za kibenki na sarafu, kuimarisha ushirikiano na wadau, pamoja na kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi na kanuni za mazingira, jamii na utawala bora ili kuendeleza sekta ya fedha.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Bodi ya Bima ya Amana imepanga kufanya uchambuzi wa utoshelevu na uendelevu wa Mfuko wa Bima ya Amana; kufanya utafiti kuhusu mfumo wa kupunguza hasara katika uwekezaji wa fedha za Mfuko wa Bima ya Amana; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mfumo wa bima ya amana nchini; kuandaa Mfumo wa Kidijitali wa Madai

ya Fidia ya Mfuko wa Bima ya Amana; kujenga jengo la ofisi za Bodi; na kufanya utafiti wa uelewa wa umma kuhusu mfumo wa bima ya amana nchini.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 105.96 ikilinganishwa na shilingi bilioni 80.61 mwaka 2025; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 43.15 kutoka shilingi bilioni 35.45 mwaka 2025; kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 330; kuongeza thamani ya mali za Benki kufikia shilingi trilioni 1.50 kutoka shilingi trilioni 1.29 mwaka 2025; na kufuatilia marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja ya shilingi bilioni 180.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Maendeleo TIB imepanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 50.71 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19.19 mwaka 2025; kuongeza mali za Benki kufikia shilingi bilioni 477.7 kutoka shilingi bilioni 280 mwaka 2025; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya Benki shilingi bilioni 41.94 na mikopo iliyoko katika mizania ya Benki shilingi bilioni 27.6.

**119. Mheshimiwa *Spika,*** Benki ya Biashara Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 243.62; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 79.00; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,844; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 2,100; kukuza mali za Benki hadi shilingi bilioni 2,762 kutoka bilioni 2,277.88 mwaka 2025; kukuza mtaji wa Benki hadi shilingi bilioni 241; na kuongeza

idadi ya wateja hadi 1,214,059 kutoka wateja 1,022,332 mwaka 2025.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF umepanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 48 ikilinganishwa na shilingi bilioni 43.25 mwaka 2025; kukuza faida kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 1.14 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.06 mwaka 2025; kukuza mtaji kutoka shilingi bilioni 59.57 mwaka 2025 hadi shilingi bilioni 61.0; kuongeza idadi ya wateja kutoka wateja 38,545 mwaka 2025 hadi wateja 48,000; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya Mfuko kutoka shilingi bilioni 3.14 mwaka 2025 hadi shilingi bilioni 3.20 na marejesho ya mikopo iliyo ndani ya mizania kutoka shilingi bilioni 51.45 mwaka 2025 hadi shilingi bilioni 53.57; na kuzalisha mapato ya jumla ya shilingi

bilioni 12.56 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.71 mwaka 2025.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi ya UTT AMIS itaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati unaotarajiwa kuongeza rasilimali za mifuko kutoka shilingi bilioni 4,847.10 mwaka 2025 hadi shilingi bilioni 6,168.75 mwaka 2026; kuongeza idadi ya wawekezaji kutoka 630,000 hadi 700,000 na kuongeza faida kabla ya kodi kutoka shilingi bilioni 46.63 hadi shilingi bilioni 63.96.

### 5.3.3 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imepanga kuendelea kuimarisha utendaji wa moduli kuu sita (6) za mfumo wa NeST pamoja na moduli zake saidizi kwa

kujumuisha matumizi ya teknolojia ya Akili Unde (AI) na kuimarisha usalama wa mfumo; kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake kwa taasisi 994 na ukaguzi wa thamani halisi ya fedha kwa taasisi 202; na kuwajengea uwezo wadau 3,450 kutoka taasisi nunuzi, 500 kutoka sekta binafsi na 1,200 kutoka makundi maalum kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake pamoja na matumizi sahihi ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi imepanga kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi 200; kusajili wataalamu 3,000 wa ununuzi na ugavi; kudahili na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa

watahiniwa 4,000; kuendesha mafunzo endelevu ya kitaaluma kwa wataalamu 5,000 wa ununuzi na ugavi; na kuendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Usajili wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Mtandaoni Toleo la II (ORS).

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma kwa upande wake imepanga kusajili na kushughulikia rufaa 55 na maombi matano (5); kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya Kuwasilisha na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa kupitia Mfumo wa NeST kwa wazabuni 400 pamoja na wakuu wa idara na vitengo vya ununuzi, TEHAMA na sheria 600; na kuboresha Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko kupitia Mfumo wa NeST.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini umepanga kukamilisha ujenzi wa ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika wilaya ya Korogwe (Tanga), Mbarali (Mbeya), na Masasi (Mtwara), kuendelea na ujenzi wa ofisi ya mkoa wa Dar es Salaam, kuwezesha Wakala kupata ithibati ya kimataifa katika utoaji wa huduma "ISO Certified", na kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kujazia Gesi (CNG) kwa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, na Dodoma. Aidha, Wakala umepanga kukamilisha kazi ya uboreshaji wa mfumo wa GIMIS kuweza kutoa huduma ya mafuta kwa mfumo wa kadi na ubadilishanaji wa taarifa kati ya mfumo wa GIMIS na mifumo ya MUSE na GAMIS. Vilevile, mfumo utaboreshwa kuwezesha madirisha maalum ya ukaguzi (*audit*) na ufuatiliaji na tathmini.

### 5.3.4 Usimamizi wa Bima Tanzania

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imepanga kusajili watoa huduma za bima 2,536 kupitia Mfumo wa Usajili Mtandaoni wa TIRA (*TIRA Online Registration System - ORS*) na Mfumo wa Ndani wa Uchakataji wa Leseni – IRS; kuendelea kuboresha Mfumo Jumuishi wa Udhibiti wa Bima (*Insurance Regulatory Integrated System – IRIS*) kwa kuongeza teknolojia ya uchambuzi wa takwimu (*Predictive Analytics*) na kuimarisha usimamizi wa usalama wa mifumo; kufanya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa sheria kwa wasajili wa bima (*insurance registrants*) 618; kufanya tafiti mbili (2) kuhusu mwenendo wa soko la bima nchini; na kutoa elimu ya bima kwa umma kwa watu milioni 27.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Bima la Taifa limepanga kuzalisha faida ghafi ya shilingi bilioni 86.31 na kufanya mapitio ya bidhaa nane (8) za bima za mali na ajali pamoja na bidhaa tatu (3) za bima za maisha ili kuendena na mahitaji ya soko. Aidha, Shirika limepanga kufanya maboresho ya vituo viwili (2) vya kuhifadhi data na urejeshaji huduma ili kuhakikisha huduma zinaendelea kupatikana pindi majanga yanapotokea.

### 5.3.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Soko la Bidhaa

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji kwa kuwafikia wananchi zaidi ya milioni 15;

kuongeza bidhaa mpya nane (8); kuendesha mafunzo yanayotambulika kimataifa kwa watendaji 1,253 wa masoko ya mitaji; na kuboresha mifumo ya kidijiti inayowezesha wateja na watoa huduma kununua na kuuza bidhaa za masoko ya mitaji kwa njia ya mtandao.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Soko la Bidhaa Tanzania limepanga kufanya mauzo ya bidhaa 12 ikiwemo ufuta, dengu, choroko, mbaazi, soya, kakao, madini, kahawa, korosho, chai, mifugo, mwani, mkonge na kuimarisha Mfumo wa Mauzo (*Online Trading System*) ili kuongeza wigo wa bidhaa zinazouzwa katika Soko la Bidhaa.

### 5.3.6 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi 21,838 katika ngazi ya astashahada, stashahada, shahada ya uzamili na uzamivu; kuendeleza jumla ya watumishi 38 ikiwemo ngazi ya shahada wanne (4), shahada ya uzamili 14 na shahada ya uzamivu 20; kufanya tafiti 28; kutoa machapisho ya kitaaluma 200; na kutoa huduma elekezi 12.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi 16,525 katika ngazi ya astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili, kuendeleza watumishi 13 katika shahada ya uzamili na 45 katika shahada

ya uzamivu, kufanya tafiti 10 na kutoa huduma elekezi sita (6). Aidha, Chuo kimepanga kutekeleza miradi ya maendeleo ya ujenzi ikiwemo kukamilisha Jengo la Taaluma katika eneo la Miyuji Kampasi Kuu ya Dodoma na kukamilisha ujenzi wa Jengo la Bweni Awamu ya Pili Kampasi ya Kanda ya Ziwa, Mwanza.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Uhasibu Arusha kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi 25,420 katika ngazi mbalimbali, kuendeleza watumishi 124 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu, kufanya tafiti nane (8) na kutoa huduma elekezi tano (5). Aidha, chuo kimepanga kuendelea na ujenzi wa jengo la Kitivo cha Fedha na Uhasibu, ujenzi wa jengo la Kitivo cha Usimamizi wa Biashara, ujenzi wa jengo la *multipurpose hall*, na ujenzi wa mabweni katika kampasi ya Dodoma na Songea.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Uhasibu Tanzania imepanga kudahili jumla ya wanafunzi 41,500 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 102 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti 18; kutoa huduma elekezi 15; na kuendelea na ujenzi wa jengo la taaluma na bweni la wanafunzi katika kampasi ya Zanzibar.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi 2,933 katika ngazi na fani mbalimbali; kuendeleza watumishi 23 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu; kufanya tafiti tano (5); na kutoa huduma elekezi nne (4).

### 5.3.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga kuendelea kuzalisha takwimu za msingi za kijamii, kiuchumi na mazingira; kufanya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2026; kufanya Utafiti wa Ajira na Mapato kwenye Sekta Rasmi wa mwaka 2026; kufanya Utafiti wa Kufuatilia Kaya wa Mwaka 2026; kuunganisha mifumo 50 ya taarifa za kiutawala kati ya taasisi na taasisi; kuunganisha mifumo 30 inayozalisha takwimu na Mfumo Jumuishi wa Kitakwimu; kuanzisha Kituo cha Kuchakata Data; kufanya Utafiti wa Mwaka wa Uzalishaji Viwandani wa Mwaka 2025; na kukamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi katika mkoa wa Pemba, Lindi na Simiyu.

### 5.3.8 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imepanga kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 400 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 15,850; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 90; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 90 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa watahiniwa 17,250; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu 1,950 wenye sifa za nje wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji nchini; kutoa mafunzo

ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 170; kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa taarifa za uendelevu katika sekta ya umma na binafsi kwa wahitimu 120; kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa taarifa za ukaguzi kwa wakaguzi wa ndani wasiokuwa na taaluma ya uhasibu kwa wahitimu 120; kutoa ushauri wa kiufundi katika matumizi ya viwango vya uhasibu, ukaguzi katika uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa kampuni 10 na kukamilisha maandalizi ya mtaala mpya wa taaluma ya uhasibu na ukaguzi.

### 5.3.9 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha

Tanzania imepanga kutoa leseni 10,021 ikijumuisha leseni mpya 6,616 na kuhuisha leseni 3,405; kufanya kaguzi 18 kwa kuzingatia vihatarishi kwenye uzingatiaji wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha na kaguzi 10 kwenye uzingatiaji wa Sheria ya Kuzuia Utakasishaji Fedha Haramu; kutekeleza operesheni nne (4) za kudhibiti michezo haramu ya kubahatisha; kukusanya jumla ya mapato ya shilingi bilioni 32.30; kuelimisha jamii kuhusu athari hasi za michezo ya kubahatisha; na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

### 5.3.10 Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi Katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, taasisi, wakala wa Serikali na

mashirika yaliyochini ya Wizara ya Fedha yanatarajiwa kuchangia shilingi 398.20 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikiwa ni mapato yasiyo ya kodi. Kati ya kiasi hicho, gawio ni shilingi bilioni 363.00, mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 12.17 na mapato mengine shilingi bilioni 13.03.

## 6.0 MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA NA FUNGU LA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA 2026/27.

### 6.1 Makadirio ya Mapato (Kodi, Maduhuli, Misaada na Mikopo)

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Wizara ya Fedha imekadiriwa kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 55,224.29. Kati ya kiasi hicho, mapato ya

kodi na yasiyo ya kodi yanayotarajiwa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ni shilingi bilioni 39,094.72. Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 23.54 na kutafuta misaada ya shilingi bilioni 563.14 pamoja na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 15,542.89. Kati ya mikopo inayotarajiwa kupatikana, mikopo yenye masharti nafuu ni shilingi bilioni 6,554.78, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 2,430.37 na mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 6,557.74. Aidha, Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linakadiriwa kukusanya shilingi milioni 485.33 ikiwa ni ukodishaji wa kumbi za mikutano na kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.1**.

**Kielelezo Na.1: Makadirio ya Mapato ya Serikali Yatakayokusanywa na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi - NAOT kwa Mwaka 2026/27**

**MAKADIRIO YA MAPATO**
**(KODI, MADUHULI, MISAADA NA MIKOPO)**
**KWA MWAKA 2026/27**

| CHANZO CHA MAPATO | KIASI (Bilioni TZS) | MHUSIKA |
|---|---|---|
| Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi | 39,094.72 | TRA |
| Mikopo ya Ndani yenye Masharti ya Kibiasahara | 6,557.74 | FUNGU 021 |
| Mikopo ya Nje yenye Masharti Nafu | 6,554.78 | FUNGU 021 |
| Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiasahara | 2,430.37 | FUNGU 021 |
| Misaada kutoka Nje | 563.14 | FUNGU 021 |
| Maduhuli ya Ndani | 23.54 | FUNGU 023 & FUNGU 050 |
| **JUMLA KUU** | **55,224.29** | |

TAX. KODI ZA KUMBI ZA MIKUTANO NA PANGO – FUNGU 045: **485.33** (Bilioni TZS)

## 6.2 Makadirio ya Matumizi ya Mafungu ya Wizara kwa Mwaka 2026/27

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Wizara ya Fedha inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 21,335.98 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu manane

(8) ya Wizara. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 19,446.89 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,889.09 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, ninaomba Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 132.22 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 120.39 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.83 matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi kwa mafungu manane (8) ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi umeoneshwa katika **Kielelezo Na.2**.

**Kielelezo Na.2: Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2026/27**

**BAJETI YA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

**MWAKA 2026/27**

**WIZARA YA FEDHA**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA (TZS) | MATUMIZI YA MAENDELEO (TZS) | JUMLA KUU (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 001 | Deni la Serikali | 14,712,796,574,000 | 0 | 14,712,796,574,000 |
| 006 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 13,991,762,000 | 1,141,967,000 | 15,133,729,000 |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 5,122,155,000 | 958,949,000 | 6,081,104,000 |
| 013 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 5,162,443,000 | 0 | 5,162,443,000 |
| 021 | Hazina | 1,311,710,828,000 | 1,699,483,142,000 | 3,011,193,970,000 |
| 022 | Huduma za Mfuko Mkuu | 3,148,637,985,000 | 0 | 3,148,637,985,000 |
| 023 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 79,216,318,000 | 6,241,381,000 | 85,457,699,000 |
| 050 | Wizara ya Fedha | 170,249,506,000 | 181,271,712,000 | 351,521,218,000 |
| JUMLA KUU MAFUNGU YA WIZARA | | 19,446,887,571,000 | 1,889,097,151,000 | 21,335,984,722,000 |

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT)**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA (TZS) | MATUMIZI YA MAENDELEO (TZS) | JUMLA KUU (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 120,396,661,000 | 11,828,000,000 | 132,224,661,000 |
| JUMLA KUU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI | | 120,396,661,000 | 11,828,000,000 | 132,224,661,000 |

| JUMLA KUU WIZARA YA FEDHA | + | JUMLA KUU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI | = | JUMLA KUU KWA PAMOJA |
|---|---|---|---|---|
| 21,335,984,722,000 | | 132,224,661,000 | | 21,468,209,383,000 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

## 7.0 HITIMISHO

***141. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2025/26 na Mpango na Bajeti ya mwaka 2026/27, naomba kutumia tena nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote waliosaidia kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa

mwaka 2025/26 na maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2026/27. Kwa namna ya pekee, ninapenda kuishukuru familia yangu – wazee, ndugu na jamaa kwa upendo, uvumilivu, maombi na faraja wanayonipa wakati wote katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nawashukuru sana kwa imani yao na moyo wa upendo. Nami nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema na baraka zaidi.

***142. Mheshimiwa Spika***, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nitahitimisha hoja yangu bila ya kuwashukuru Naibu Mawaziri wangu Mheshimiwa *Mhandisi* Mshamu Ali Munde (Mb,) na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula (Mb,) kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha,

nawashukuru watendaji wakuu wa wizara wakiongozwa na *Dkt*. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bw. Elijah G. Mwandumbya, Bw. Nsubili A. K. Joshua na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Bi. Amina Kh. Shaaban kwa ushauri wao na usimamizi makini wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo, wasaidizi wa Ofisi ya Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa.

***143. Mheshimiwa Spika***, pia nawashukuru kwa dhati wakuu na watumishi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, CPA(T).

Yusuph Juma Mwenda kwa utekelezaji thabiti wa majukumu yao na ushirikiano wao katika utendaji kazi. Kwa namna ya pekee, na kwa dhati ya moyo wangu, namshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu yangu CPA(T). Charles Edward Kichere pamoja na watumishi wote wa Ofisi yake kwa kazi nzuri ya ukaguzi wa matumizi ya rasilimali za umma wanayoendelea kuifanya. Taarifa zake na ushauri wa hatua za kuchukua zimekuwa ni msingi wa kuboresha usimamizi wa fedha na mali za umma nchini.

***144. Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb,), Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ali Hassan King (Mb,), wajumbe wa Kamati, makatibu wa Kamati na

watumishi wote wa Ofisi ya Bajeti ya Bunge kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchambua mapendekezo ya fungu moja moja na hatimaye kuridhia yawasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninawaahidi kuendelea kushirikiana nao katika hatua ya utekelezaji wa mapendekezo ya mpango na bajeti hii mara baada ya kuidhinishwa na Bunge.

***145. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa michango yao ya hali na mali katika kufanikisha mipango ya Wizara na Taifa kwa ujumla. Michango yao ya kifedha na kitaalamu imewezesha kufikiwa shabaha katika kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria, kitaasisi na kiutendaji. Aidha, fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya

maendeleo zimesaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

***146. Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, ninapenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Niwashukuru waheshimiwa wabunge na umma wa watanzania kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

***147. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho Na.1: Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Mishahara hadi Aprili 2026**

MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA

# BAJETI YA MISHAHARA

hadi APRILI 2026

TZS

## BAJETI YA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA

| JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|
| 006 - Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 2,366,512,000.00 | 2,366,512,000.00 | 1,895,585,700.00 | 1,894,976,799.00 | 99.97% |
| 010 - Tume ya Pamoja ya Fedha | 945,493,000.00 | 945,493,000.00 | 708,255,020.00 | 708,255,020.00 | 100.00% |
| 021 - Hazina | 985,183,709,000.00 | 664,880,946,898.39 | 447,888,970,925.25 | 447,835,411,623.08 | 99.99% |
| 022 - Huduma za Mfuko Mkuu | 16,616,460,000.00 | 16,616,460,000.00 | 9,253,260,270.20 | 9,253,260,270.20 | 100.00% |
| 023 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 7,468,014,000.00 | 7,468,014,000.00 | 7,150,653,504.00 | 7,150,446,004.00 | 100.00% |
| 050 - Wizara ya Fedha | 89,011,587,000.00 | 89,011,587,000.00 | 75,272,903,317.28 | 67,921,078,455.27 | 90.23% |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA - PE** | **1,101,591,775,000.00** | **781,289,012,898.39** | **542,169,628,736.73** | **534,763,428,171.55** | **98.63%** |

## OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT)

| JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|
| 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 23,058,129,000.00 | 23,058,129,000.00 | 18,025,524,639.90 | 18,025,524,639.90 | 100.00% |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE - PE** | **1,124,649,904,000.00** | **804,347,141,898.39** | **560,195,153,376.63** | **552,788,952,811.45** | **98.68%** |

**Kiambatisho Na.2: Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo hadi Aprili 2026**

MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA

# BAJETI YA MATUMIZI MENGINEYO

hadi APRILI 2026

TZS

## BAJETI YA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA

| JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|
| 001 - Deni la Serikali | 14,219,350,702,000.00 | 14,069,350,702,000.00 | 9,752,328,014,748.92 | 9,752,262,212,944.09 | 100.00% |
| 006 - Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 11,430,429,000.00 | 11,430,429,000.00 | 10,286,556,166.31 | 10,111,191,451.89 | 98.30% |
| 010 - Tume ya Pamoja ya Fedha | 4,164,536,000.00 | 4,164,536,000.00 | 3,285,145,234.67 | 2,882,044,985.90 | 87.73% |
| 013 - Kitenge cha Kudhibiti Fedha Haramu | 5,162,443,000.00 | 6,955,591,171.00 | 5,663,305,859.57 | 5,335,627,375.54 | 94.21% |
| 021 - Hazina | 783,658,931,000.00 | 1,238,352,161,354.41 | 1,158,493,173,913.24 | 1,158,436,801,490.45 | 100.00% |
| 022 - Huduma za Mfuko Mkuu | 3,131,303,648,000.00 | 3,131,303,648,000.00 | 2,024,354,493,991.27 | 2,005,469,909,725.06 | 99.07% |
| 023 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 91,566,300,000.00 | 130,746,300,000.00 | 104,318,534,605.00 | 101,208,771,872.00 | 97.02% |
| 050 - Wizara ya Fedha | 80,571,827,000.00 | 80,571,827,000.00 | 64,829,083,244.98 | 64,008,428,385.01 | 98.73% |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA - OC** | **18,327,208,816,000.00** | **18,672,875,194,525.40** | **13,123,558,307,764.00** | **13,099,714,988,229.90** | **99.82%** |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE - OC** | **18,414,565,810,000.00** | **18,772,091,687,525.40** | **13,215,425,802,764.00** | **13,184,302,733,729.90** | **99.76%** |

## OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT)

| JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|
| 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 87,356,994,000.00 | 99,216,493,000.00 | 91,867,495,000.00 | 84,587,745,500.00 | 92.08% |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE - OC** | **18,414,565,810,000.00** | **18,772,091,687,525.40** | **13,215,425,802,764.00** | **13,184,302,733,729.90** | **99.76%** |

**Kiambatisho Na.3: Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti Maendeleo hadi Aprili 2026**

## MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI MAENDELEO hadi APRILI 2026


TZS

### BAJETI YA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA – MAENDELEO

| JINA LA FUNGU | CHANZO CHA FEDHA | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 006 - Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | Ndani | 141,967,000.00 | 141,967,000.00 | 141,967,000.00 | 0 | – |
| | Nje | 1,136,430,000.00 | 1,136,430,000.00 | 1,136,430,000.00 | 991,072,197.39 | 87.21% |
| 010 - Tume ya Pamoja ya Fedha | Ndani | 958,949,000.00 | 958,949,000.00 | 0 | 0 | – |
| | Nje | 0 | 0 | 0 | 0 | – |
| 021 - Hazina | Ndani | 588,911,977,000.00 | 406,376,118,121.11 | 384,945,557,237.11 | 384,602,764,552.68 | 99.91% |
| | Nje | 101,824,470,000.00 | 21,256,065,400.00 | 6,569,993,003.28 | 6,546,785,277.76 | 99.65% |
| 023 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Ndani | 741,381,000.00 | 741,381,000.00 | 741,381,000.00 | 0 | – |
| | Nje | 4,090,081,000.00 | 4,090,081,000.00 | 2,456,788,000.00 | 2,406,329,115.00 | 97.95% |
| 050 - Wizara ya Fedha | Ndani | 10,946,552,000.00 | 21,301,552,000.00 | 7,522,251,541.78 | 6,890,822,964.29 | 91.61% |
| | Nje | 38,544,967,000.00 | 29,989,967,000.00 | 13,871,754,080.46 | 13,849,241,115.46 | 99.84% |
| Jumla - Maendeleo Ndani | | 601,700,826,000.00 | 429,519,967,121.11 | 393,351,156,778.89 | 391,493,587,516.97 | 99.53% |
| Jumla - Maendeleo Nje | | 145,595,948,000.00 | 56,472,543,400.00 | 24,034,965,083.74 | 23,793,427,705.61 | 99.00% |
| JUMLA MAFUNGU YA WIZARA – MAENDELEO | | 747,296,774,000.00 | 485,992,510,521.11 | 417,386,121,862.63 | 415,287,015,222.58 | 99.50% |

### OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT)

| JINA LA FUNGU | CHANZO CHA FEDHA | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2025/26 | BAJETI ILIYOHUISHWA | FEDHA ZILIZOTOLEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | % YA UFANISI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | Ndani | 8,828,000,000.00 | 8,828,000,000.00 | 6,783,535,024.66 | 6,072,688,088.20 | 89.52% |
| | Nje | 3,275,996,000.00 | 3,275,996,000.00 | 2,243,250,000.00 | 2,243,250,000.00 | 100.00% |
| Jumla Kuu - Maendeleo | | 759,400,770,000.00 | 498,096,506,521.11 | 426,412,906,887.29 | 423,602,953,310.78 | 99.77% |


Wizara ya Fedha
Dodoma